02

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

OCGS

TAKWIMU KWA MAENDELEO

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR

## FEBRUARI, 2025

MAHKAMA YA ZANZIBAR – THE JUDICIARY OF ZANZIBAR

SMZ CHUO CHA MAFUNZO – UONGOZI NA KAZI

Funded by the European Union

UN WOMEN – United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women

**25 MACHI, 2025**

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWEZI WA FEBRUARI, 2025

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa kuimarisha takwimu za jinsia nchini ikiwemo kukusanya na kuchambua takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukioyaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu 21.

## LENGO


Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera nawatoa maamuzi.

## MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA

Jumla ya matukio 107 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Februari, 2025 ambapo waathirika walikuwa 108. Waathirika wengi walikuwa watoto sawa na asilimia 80.6, wakifuatiwa na wanawake asilimia 17.6 na wanaume asilimia 1.9.


Miongoni mwa watoto (waathirika 87), wasichana walikuwa 78 (asilimia 89.7) na wavulana walikuwa 9 (asilimia 10.3).

**Kielelezo 1.1: Idadi ya Waathirika wa Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Februari 2025**




Idadi ya Matukio ya kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 52, ambapo waathirika 46 wasichana na sita (6) wanawake. Matukio ya kulawiti yalikuwa 8 na kujaribu kulawiti moja (1) ambapo waathirika wote tisa (9) walikuwa wavulana. Matukio ya kuingilia kinyume na maumbile yalikuwa matano (5) ambapo waathirika wawili (2) wanawake na watatu (3) wasichana. Matukio ya kutorosha ni 19 ambapo waathirika 18 wasichana na mmoja mwanamke. Matukio ya shambulio la aibu/kukashifu yalikuwa 15 kati ya hayo waathirika 10 wasichana na watano (5) wanawake. Matukio ya mauaji yalikuwa mawili (2) ambapo waathirika wote walikuwa wanaume. Tukio la kutupa watoto lililoripotiwa lilikuwa moja, ambapo muathirika alikuwa ni msichana. Matukio ya kumpa na kupokea ujauzito yalikuwa mawili (2) ambapo waathirika wote walikuwa wanawake.

**Kielelezo 1.2 Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Aina ya Matukio, Februari, 2025**




Wilaya ya Magharibi ‘A’ imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 25) sawa na asilimia 23.4 ikifuatia wilaya ya Magharibi ‘B’ ambapo yameripotiwa matukio 24 (asilimia 22.4). Wilaya ya Kusini na Micheweni zimeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio, matukio matatu (3) sawa na asilimia 2.8 kwa kila wilaya.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Februari, 2025**



Idadi ya matukio kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 38.9 kufikia matukio 107 kwa mwezi Februari, 2025 kutoka matukio 175 kwa mwezi wa Februari, 2024. Matukio yote yameripotiwa kupungua kwa mwezi Februari, 2025 isipokuwa tukio la Kutorosha limeongezeka. Wilaya ya Magharibi 'A' ina idadi kubwa ya matukio kwa Februari, 2025 (matukio 25) na wilaya ya Magharibi 'B' ilikuwa na idadi kubwa ya matukio kwa mwezi wa Februari, 2024 (matukio 43).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya na Aina ya udhalilishaji, Februari 2024 na Februari, 2025**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti/Kunajisi | | Kujaribu kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | |
| | Feb-24 | Feb-25 | Feb-24 | Feb-25 | Feb-24 | Feb-25 | Feb-24 | Feb-25 | Feb-24 | Feb-25 | Feb-24 | Feb-25 |
| Kaskazini 'A' | 4 | 10 | 1 | 8 | 0 | 0 | | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 13 | 5 | 9 | 5 | 1 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 8 | 5 | 5 | 4 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kusini | 5 | 3 | 3 | 2 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Mjini | 39 | 12 | 15 | 7 | 3 | 3 | | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Magharibi 'A' | 39 | 25 | 14 | 10 | 2 | 1 | | 0 | 3 | 3 | 3 | 2 |
| Magharibi 'B' | 43 | 24 | 21 | 8 | 4 | 1 | | 0 | 3 | 2 | 5 | 13 |
| Wete | 8 | 6 | 6 | 1 | 0 | 1 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 3 | 2 | 2 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 9 | 8 | 4 | 1 | 1 | 1 | | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 |
| Mkoani | 5 | 6 | 4 | 4 | 0 | 1 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **175** | **107** | **84** | **52** | **11** | **8** | | **1** | **6** | **5** | **14** | **19** |

Inaendelea.... **Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya na Aina ya udhalilishaji, Februari 2024 na Februari, 2025**

| Wilaya | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Lugha ya matusi | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Mauaji | | Kutupa Watoto | | Kumpa na Kupokea ujauzito | |
| | Feb-24 | Feb-25 | Feb-24 | Feb-25 | Feb-24 | Feb-25 | Feb-24 | Feb-25 | Feb-24 | Feb-25 | Feb-24 | Feb-25 |
| Kaskazini 'A' | | 0 | 1 | 1 | 0 | | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kaskazini 'B' | | 0 | 3 | 0 | 0 | | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kati | | 0 | 2 | 0 | 0 | | | 0 | | 1 | | 0 |
| Kusini | | 0 | 2 | 0 | 0 | | | 0 | | 0 | | 0 |
| Mjini | | 0 | 3 | 2 | 16 | | | 0 | | 0 | | 0 |
| Magharibi 'A' | | 0 | 5 | 7 | 12 | | | 2 | | 0 | | 0 |
| Magharibi 'B' | | 0 | 1 | 0 | 9 | | | 0 | | 0 | | 0 |
| Wete | | 2 | 2 | 0 | 0 | | | 0 | | 0 | | 2 |
| Micheweni | | 0 | 0 | 1 | 0 | | | 0 | | 0 | | 0 |
| Chake Chake | | 0 | 3 | 3 | 0 | | | 0 | | 0 | | 0 |
| Mkoani | | 0 | 1 | 1 | 0 | | | 0 | | 0 | | 0 |
| **Jumla** | | **2** | **23** | **15** | **37** | | | **2** | | **1** | | **2** |

Miongoni mwa watoto 87 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Wasichana waliobakwa walikuwa 46, Wavulana waliolawitiwa walikuwa 8, wavulana waliojaribu kulawitiwa alikuwa mmoja, Kuingilia kinyume na maumbile walikuwa wasichana watatu (3), Kutorosha walikuwa wasichana 18, shambulio la aibu/kukashifu wasichana 10 na kutupa watoto msichana mmoja.

**Jadweli 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto, Wilaya na Aina ya Matukio Februari, 2025**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kujaribu kubaka | Kulawiti/ Kunajisi | Kujaribu kulawiti/ Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Kutupa Watoto | |
| | | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 9 | 6 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kusini | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 9 | 6 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 17 | 9 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 22 | 7 | 0 | 1 | 0 | 2 | 12 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 2 | 1 | 0 | 1 | | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 8 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 6 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **87** | **46** | **0** | **8** | **1** | **3** | **18** | **0** | **10** | **0** | **1** | **0** |

Miongoni mwa waathirika wanawake 19 wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; waliobakwa walikuwa sita (6), kuingilia kinyume na maumbile wawili (2), kutorosha alikuwa mmoja, lugha ya matusi watatu (3), shambulio la aibu au kukashifu watano (5) na kumpa na kupokea ujauzito wawili (2).

**Jadweli 1.4a: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya Februari, 2025**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kujaribu kubaka | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Lugha ya matusi | Shambulio la aibu/Kukashifu | Kumpa na Kupokea ujauzito |
| Kaskazini 'A' | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Magharibi 'A' | 6 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 3 | 0 |
| Magharibi 'B' | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 |
| Micheweni | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **19** | **6** | **0** | **2** | **1** | **3** | **5** | **2** |

Kwa mwezi wa Februari 2025, Jumla ya matukio wawili (2) ya mauaji yaliripotiwa kwa wanaume, ambapo wote wameripotiwa kutoka Wilaya ya Magharibi A.

**Jadweli 1.4b: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya Februari, 2025**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti/Kunajisi | Kujaribu kulawiti/Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Lugha ya matusi | Shambulio la aibu/Kukashifu | Kutelekeza Mtoto | Kuingilia maharimu | Mauaji |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **2** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **2** |

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 58) sawa na asilimia 66.7 ya matukio yote ya watoto yaliyoripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 11) sawa na asilimia 12.6. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17 (matukio 40) sawa na asilimia 87.0 kati ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

Jadweli 1.5: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto na Umri Februari, 2024

| Umri | 0-5 | | 6-10 | | 11-14 | | 15-17 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jinsi | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kubaka | 2 | | 2 | | 2 | | 40 | |
| Kujaribu Kubaka | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 3 | | 3 | | 2 | | 1 |
| Kujaribu kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | | 1 | | 1 | | 1 | |
| Kutorosha | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 15 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 3 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 |
| Kutupa Watoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla ya Waathirika** | **6** | **3** | **6** | **3** | **9** | **2** | **57** | **1** |


Idadi ya matukio ya watoto kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 40.4 kufikia matukio 87 kwa mwezi wa Februari 2025 kutoka matukio 146 kwa mwezi wa Februari 2024. Matukio yote yameripotiwa kupungua kwa mwezi Februari 2025 kutoka Februari 2024 isipokuwa matukio ya Kutorosha yameongezeka.

**Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri na Aina ya Matukio, Mwezi Februari, 2024 na Februari, 2025**

| | Kubaka | | Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Kutupa Watoto | | Shambulio | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Miaka** | **24-Feb** | **25-Feb** | **24-Feb** | **25-Feb** | **24-Feb** | **25-Feb** | **24-Feb** | **25-Feb** | **24-Feb** | **25-Feb** | **24-Feb** | **25-Feb** | **24-Feb** | **25-Feb** | **24-Feb** | **25-Feb** |
| 0-5 | 4 | 2 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 3 | | 1 | 0 | | 8 | 9 |
| 6-10 | 8 | 2 | 5 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 4 | 3 | | 0 | 4 | | 22 | 9 |
| 11-14 | 20 | 2 | 4 | 2 | 2 | 1 | 2 | 3 | 4 | 3 | | 0 | 8 | | 40 | 11 |
| 15-17 | 47 | 40 | 1 | 1 | 1 | 1 | 8 | 15 | 8 | 1 | | 0 | 11 | | 76 | 58 |
| **Jumla** | **79** | **46** | **11** | **9** | **4** | **3** | **10** | **18** | **19** | **10** | | **1** | **23** | | 146 | 87 |

Matukio mengi (matukio 52) yametokea nyumbani kwa mtuhumiwa sawa na asilimia 48.6 ikifuatiwa na idadi ya matukio yaliyotokea sehemu nyengine (matukio 18) sawa na asilimia 16.8 ikilinganishwa na maeneo mengine yaliyoripotiwa kwa mwezi Februari 2025.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea Februari, 2025**




Matukio 105 kati ya matukio 107 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 98.1 ya matukio yote yaliyoripotiwa aidha matukio mawili yamefungwa na polisi( asilimia 1.9). Matukio mawili (2) yaliyoripotiwa ya kubaka yamefungwa na polisi.

**Jadweli 1.8: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa Februari, 2025**

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | Waathirika | | Waathirika | | Hatua Zilizofikia | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Watoto | | Watu Wazima | | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwa huru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Ofisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi | Hati ya Mashtaka |
| | | Wasichana | Wavulana | W'ke | M'me | | | | | | | |
| Kubaka | 52 | 46 | | 6 | | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 50 | 0 |
| Kujaribu Kubaka | 0 | 0 | | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kulawiti/Kunajisi | 8 | | 8 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 | 0 |
| Kujaribu kulawiti/Kunajisi | 1 | | 1 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 5 | 3 | | 2 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 |
| Kutorosha | 19 | 18 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 19 | 0 |
| Lugha ya matusi | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 15 | 10 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 15 | 0 |
| Mauaji | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Kutupa Watoto | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| **Jumla** | **107** | **78** | **9** | **19** | **2** | **0** | **0** | **0** | **2** | **0** | **105** | **0** |

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia walioripotiwa mwezi wa Februari 2025 walikuwa 107 kati yao 54 walikuwa wapenzi sawa na asilimia 50.5, watu wasiojulikana walikuwa 34 sawa na asilimia 31.8 , watu wengine walikuwa 11 na jirani saba (7)

**Kielelezo 1.5: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia Februari, 2025**



## MAJALADA YA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOPOKELEWA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA ZANZIBAR FEBRUARI, 2025

Jumla ya Majalada 31 yamepokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwezi wa Februari, 2025 ambayo yalihusisha makosa 31.

Idadi kubwa ya makosa yaliyopokelewa yametokea Mkoa wa Mjini Magharibi (makosa 16) sawa na asilimia 51.6 ya makosa yote ikilinganishwa na mikoa mwengine.

**Jadweli 2.1: Idadi ya Majalada na Mkosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa Februari,2025**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Idadi ya Makosa |
|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 0 | 0 |
| Kusini Unguja | 2 | 2 |
| Mjini Magharibi | 16 | 16 |
| Kaskazini Pemba | 4 | 4 |
| Kusini Pemba | 9 | 9 |
| Makao Makuu | 0 | 0 |
| **Jumla** | **31** | **31** |

Jumla ya Majalada 31 ya Udhalilishaji yameripotiwa kupokelewa kwa mwezi wa Februari,2025. Kati ya majalada 31 yaliyopokelewa, majalada 11 yameruhusiwa kwenda mahakamani, majalada 10 yamerudishwa Polisi kwa Upelelezi zaidi, majalada sita (6) hayajatolewa uamuzi, na majalada manne (4) yamependekezwa kufungwa.

**Jadweli 2.2 Majalada ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa na Hatua, Februari 2024**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Yalioruhusiwa kwenda Mahakamani | Yaliopendekezwa kufungwa | Yaliorudi Polisi kwa Upelelezi | Hayajatolewa Uamuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini Unguja | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Mjini Magharibi | 16 | 2 | 1 | 7 | 6 |
| Kaskazini Pemba | 4 | 1 | 1 | 2 | 0 |
| Kusini Pemba | 9 | 7 | 2 | 0 | 0 |
| Mkao Makuu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **31** | **11** | **4** | **10** | **6** |

Miongoni mwa makosa 31 ya udhalilishaji yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 21) sawa na asilimia 67.7 ya makosa yote yaliyopokelewa.

**Jadweli 2.3: Idadi ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa, Februari 2024**


| Aina ya Makosa | Kaskazini Unguja | Kusini Unguja | Mjini Magharibi | Kaskazini Pemba | Kusini Pemba | Makao Makuu | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kulawiti /Kunajisi | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | **2** |
| Kubaka kwa Kiundi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Kubaka | 0 | 2 | 12 | 2 | 5 | 0 | **21** |
| Kujaribu Kubaka | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Kukashifu/Shambulio la Aibu | 0 | 0 | 3 | 1 | 4 | 0 | **8** |
| **Idadi ya Makosa** | **0** | **2** | **16** | **4** | **9** | **0** | **31** |

## TAKWIMU ZA UDHALILISHAJI

### Takwimu za Udhalilishaji Zilizofunguliwa katika Mahakama za Udhalilishaji Zanzibar kwa Mwezi wa Februari 2025

Jumla ya mashauri 14 ambayo yanahusisha makosa 17 yamefunguliwa katika mahkama za udhalilishaji kwa mwezi wa Februari, 2025 ambapo Mkoa wa Mjini Magharibi umeripotiwa kuwa na mashauri mengi yaliyofunguliwa (mashauri 8 yanayohusisha makosa 10) sawa na asilimia 57.1 ya mashauri ikilinganishwa na mikoa mengine

**Kielelezo 3.1: Mashauri ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyofunguliwa kwa Mkoa Februari, 2025**




Jumla ya mashauri 14 yaliyofunguliwa katika Mahkama za udhalilishaji Zanzibar, mashauri 12 bado yanaendelea na mashauri mawili (2) yametiwa hatiani.

**Jadweli 3.1: Mashauri ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyofunguliwa katika Mahkama za Udhalilishaji kwa Hatua na Aina ya Kosa Februari, 2025**

| Aina ya makosa | Zilizopokelewa | Zinazoendelea | Zilizotiwa hatiani | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kifungo | Faini | Fidia | Kifungo na fidia | Faini na fidia |
| Kubaka | 6 | 6 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kubaka kwa kundi | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kubaka na kutorosha | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kubaka na kumuingilia kinyume na maumbile | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kulawiti na shambulio la aibu | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kukashifu | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **14** | **12** | **0** | **1** | **0** | **0** | **1** |

Jumla ya washtakiwa wa makosa ya vitendo vya udhalilishaji walikuwa 16 ambapo washtakiwa wote walikuwa wanaume. Washtakiwa wengi walikuwa na umri wa miaka 18-24 (washtakiwa 10 ) sawa na asilimia 62.5 ya washtakiwa wote.

Jumla ya waathirika wa vitendo vya udhalilishaji walikuwa 14 ambapo muathirika mmoja alikuwa mvulana na waathirika 12 walikuwa wasichana na muathirika mmoja mwanamke. Waathirika wengi zaidi walikuwa na umri wa miaka 15-17 (waathirika 7) sawa na asilimia 50.0 ya waathirika wote.

**Jadweli 3.2: Idadi ya Washtakiwa na Waathirika wa Vitendo vya Udhalilishaji katika Mahkama za Udhalilishaji kwa Jinsi na Umri Februari, 2025**

| Umri wa Mshtakiwa | Washtakiwa | | Umri wa Waathirika | Waathirika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | M/ME | MKE | | M/ME | MKE |
| **13-Dec** | 0 | 0 | **0-5** | 1 | 3 |
| **14-15** | 0 | 0 | **10-Jun** | 0 | 0 |
| **16-17** | 1 | 0 | **14-Nov** | 0 | 2 |
| **18-24** | 10 | 0 | **15-17** | 0 | 7 |
| **25-35** | 3 | 0 | **18-24** | 0 | 0 |
| **36-45** | 0 | 0 | **25-35** | 0 | 1 |
| **46-64** | 1 | 0 | **36-45** | 0 | 0 |
| **65+** | 1 | 0 | **46-64** | 0 | 0 |
| | | | **65+** | 0 | 0 |
| **Jumla** | **16** | **0** | **Jumla** | **1** | **13** |

## HITIMISHO

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu 21. Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 107 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Februari, 2025 ambapo waathirika walikuwa 108.  Wilaya ya Magharibi “A” imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 25) sawa na asilimia 23.1 .  Idadi ya matukio kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 38.9 na kufikia matukio 107 mwezi wa Februari, 2025 kutoka matukio 175 kwa mwezi wa Februari, 2024.

Matukio 105 kati ya matukio 107 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la  Polisi  sawa na asilimia 98.1 ya matukio yote yaliyoripotiwa aidha matukio mawili yamefungwa na polisi( asilimia 1.9).

## Kiambatanisho

**Jadweli 1.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika na Aina ya Matukio Februari, 2024**

| Sehemu Zilotokezea | Nyumbani kwa Muathirika | | Nyumbani kwa Mtuhumiwa | | Nyumba za wageni/rafiki | | Majumba mabovu | | Vichakani | | Sehemu nyengine | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **W'ke/Wasichana** | **W'me/Wavulana** | **W'ke/Wasichana** | **W'me/Wavulana** | **W'ke/Wasichana** | **W'me/Wavulana** | **W'ke/Wasichana** | **W'me/Wavulana** | **W'ke/Wasichana** | **W'me/Wavulana** | **W'ke/Wasichana** | **W'me/Wavulana** |
| Kubaka | 2 | | 32 | | 4 | | 7 | | 1 | | 6 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 2 | | 0 | | 5 | | 1 | | 0 |
| Kujaribu kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | | 5 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | |
| Kutorosha | 4 | 0 | 8 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 |
| Lugha ya matusi | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 3 | 0 | 5 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 5 | 0 |
| Mauaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Kutupa Watoto | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | **11** | **2** | **50** | **2** | **4** | **2** | **9** | **5** | **3** | **1** | **15** | **3** |

**Jadweli 2.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Februari, 2025**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kujaribu kubaka | Kulawiti/Kunajisi | Kujaribu kulawiti/Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Kutupa Watoto | |
| | | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 9 | 6 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kusini | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 9 | 6 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 17 | 9 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 22 | 7 | 0 | 1 | 0 | 2 | 12 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 8 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 6 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **87** | **46** | **0** | **8** | **1** | **3** | **18** | **0** | **10** | **0** | **1** | **0** |

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mwaka, 2024 na Februari, 2025**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Mwanamme | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Feb-24 | Feb-25 | Feb-24 | Feb-25 | Feb-24 | Feb-25 | Feb-24 | Feb-25 | Feb-24 | Feb-25 |
| Kubaka | 84 | 52 | 5 | 6 | 79 | 46 | | | | |
| Kulawiti/Kunajisi | 11 | 8 | | | | | 11 | 8 | 0 | 0 |
| Kujaribu kulawiti/Kunajisi | 0 | 1 | | | | | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 6 | 5 | 2 | 2 | 4 | 3 | | | | |
| Kutorosha | 14 | 19 | 4 | 1 | 10 | 18 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Lugha ya matusi | 0 | 2 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 23 | 15 | 5 | 5 | 19 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio | 37 | 0 | 7 | 0 | 11 | 0 | 12 | 0 | 7 | 0 |
| Mauaji | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Kutupa Watoto | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kumpa na Kupokea ujauzito | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **175** | **107** | **23** | **19** | **123** | **78** | **23** | **9** | **7** | **2** |

**Jadweli 4.0 : Idadi ya Waathirika Wanawake na Wanaume wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, kwa Umri na Aina ya Matukio; Februari 2025**

| Umri | 18-24 | | 25-35 | | 36-45 | | 46-64 | | 65+ | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** |
| **Jumla ya Waathirika** | **9** | **0** | **7** | **2** | **3** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **19** | **2** |
| Kubaka | 1 | | 4 | | 1 | | 0 | | 0 | | 6 | |
| Kujaribu Kubaka | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kujaribu kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 2 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 2 | |
| Kutorosha | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Lugha ya matusi | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 3 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 |
| Kutupa Watoto | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |

**Jadweli 5.0: Muda wa Matukio ya Udhalilishaji Yalipotokea; Februari, 2025**

| Muda Uliyotokea Matukio | 12:01 - 03:00 Asubuhi | | 03:01 - 6:00 Mchana | | 6:01 - 9:00 Jioni | | 9:01 - 12:00 Jioni | | 12:01 - 3:00 Usiku | | 3:01 - 09:00 Usiku | | 6:01 - 09:00 Usiku | | 09:01 - 12:00 Asubuhi | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke/W asicha na | W'me/ Wavula na | W'ke/W asicha na | W'me/ Wavula na | W'ke/W asicha na | W'me/ Wavula na | W'ke/W asicha na | W'me/ Wavula na | W'ke/W asicha na | W'me/ Wavula na | W'ke/W asicha na | W'me/ Wavula na | W'ke/W asicha na | W'me/ Wavula na | W'ke/W asicha na | W'me/ Wavula na | W'ke/W asicha na | W'me/ Wavul ana |
| Kubaka | 4 | | 5 | | 11 | | 17 | | 13 | | 2 | | 0 | | 0 | | 52 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 0 | | 2 | | 5 | | 1 | | 0 | | 0 | | 0 | | 8 |
| Kujaribu kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | | 0 | | 2 | | 1 | | 2 | | 0 | | 0 | | 0 | | 5 | |
| Kutorosha | 0 | 0 | 3 | 0 | 7 | 0 | 3 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 19 | 0 |
| Lugha ya matusi | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 0 | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 8 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 15 | 0 |
| Mauaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Kutupa Watoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendochochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi auya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wangono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile nashambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hiiya mwaka 2004. Sheria hii imetungwapamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenyeshehemu ya kumi na tatu (Section thirteen)ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendovya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyohaviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishajiwa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wakijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadikifungo cha maisha.

**Kwa Ufafanuzi Zaidi Tafadhali Wasiliana na:**

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua,2321,
Simu: +255242231869
Barua pepe: cgs@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.comNukushi: 024223136
**MMP, Zanzibar.**